**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO**

**MHESHIMIWA DKT. SAADA M. SALUM**

**AKIWASILISHA**

# MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI MWAKA 2025 NA MPANGO WA MAENDELEO WA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWAKA 2025/2026

# YALIYOMO


UTANGULIZI .......... 1
MAPITIO YA HALI YA UCHUMI 2024 .......... 5
Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Dunia .......... 6
Hali ya Mfumuko wa Bei Duniani .......... 7
Mapitio ya hali ya Uchumi wa Zanzibar .......... 8
Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Zanzibar .......... 10
Hali ya Ajira .......... 11
Mwenendo wa thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi Dola ya Kimarekani .......... 12
Mwenendo wa Uingiaji wa Watalii Zanzibar .......... 13
Sekta ya Nje .......... 14
Utekelezaji wa Maeneo ya Kimkakati kwa Kipindi cha Miezi Tisa (Julai 2024 -Machi 2025) .......... 17
MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI MWAKA 2025 .......... 28
MALENGO NA SHABAHA ZA UCHUMI JUMUISHI KWA MWAKA 2025 .......... 28
MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2025/2026 .......... 31
MAPENDEKEZO YA MAENEO YA KIMKAKATI KWA MWAKA 2025/2026 .......... 31
RASILIMALI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2025/2026 .......... 34
MAENEO MTAMBUKA .......... 34
Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP -2021-2026) .......... 34
Masuala ya Idadi ya watu .......... 35
Uhifadhi wa Mazingira .......... 36
Kukabiliana na Maafa .......... 37
Mapambano dhidi ya Madawa ya Kulevya .......... 37
Makundi yenye Mahitaji Maalumu .......... 38
Mipango ya Kuendeleza Watenda Kazi .......... 39
UFUATILIAJI, TATHIMINI NA UTOAJI WA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI .......... 39

MAJUMUISHO ........................................................................ 42
HITIMISHO ........................................................................ 42

## A. UTANGULIZI

1.0 **Mheshimiwa Spika,** *Kwa kuzingatia Kanuni ya 100 (1 na 2) na 106 (2) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Agosti 2024,* Kwa heshima ninaomba kutoa hoja kwamba, Baraza lako lipokee, lijadili na kushauri **Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2025/2026.** Naomba kuwasilisha Hotuba ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2025/26 inayoambatana na **Kitabu cha Kwanza cha Mapitio ya Hali ya Uchumi 2024 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 na Kitabu cha Pili cha Mwelekeo wa Hali ya Uchumi 2025 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2025/2026.**

2.0 **Mheshimiwa Spika,** Utayarishaji wa Mpango huu wa maendeleo umezingatia **Malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya Mwaka 2050; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020-2025; Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026;** Hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi aliyoitoa wakati wa **Ufunguzi wa Baraza la Kumi (10) la Wawakilishi** na ahadi anazozitoa anapokutana na wananchi katika nyakati tofauti. Vile vile, mazingatio ya mpango huu yapo katika **Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ya Mwaka 2015-2030; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika ya mwaka 2063; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ya mwaka 2050; pamoja na Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ya Mwaka 2050.** Aidha, Mpango umekwenda sambamba na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na teknolojia yanayoendelea duniani. Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo kisekta ni moja ya nyenzo zilizotumika kujua utekelezaji halisi wa Mipango ya Maendeleo kwa kubainisha mafanikio na changamoto.

3.0 **Mheshimiwa Spika,** Shukurani za pekee ziende kwa Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia neema ya uhai na afya njema iliyoniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako kwa mara nyengine kuwasilisha **Hotuba ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2025/2026** na kulijaalia Taifa letu kuwa na amani, utulivu na mshikamano na kwa kutuwezesha kukutana katika Mkutano huu wa Baraza la Kumi (10) la Wawakilishi ili kujadili namna ya kuharakisha maendeleo ya Taifa kupitia Bajeti zilizowasilishwa katika Baraza hili la kujadili Bajeti.

4.0 **Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote, na kwa namna ya pekee, ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru kwa dhati ya moyo wangu **Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi** kwa kuniamini na kuniteua kushika dhamana ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango. Hakika imani hii kwangu ni kubwa sana binafsi na wenzangu wote katika Ofisi yetu. Tutaendelea kufanya kazi kwa bidii na uadilifu wa hali ya juu, kwani tunafahamu kuwa, Ofisi yetu ni moja ya mhimili na chachu ya maendeleo yote tunayoyaona hapa nchini.

5.0 **Mheshimiwa Spika,** Maono ya **Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi** ya kuleta Mapinduzi katika tasnia ya uchumi yenye kuchochea ukuaji wa uchumi wa Zanzibar, pamoja na kuongezeka kwa mashirikiano baina ya nchi yetu na nchi rafiki, kuvutia wawekezaji binafsi na kuimarisha mazingira ya uwekezaji kwa kuitangaza nchi yetu kuwa kivutio na mahala salama kutembelea na kuwekeza. Miongoni mwa shughuli alizozisimamia kwa nguvu zake zote ni pamoja na uimarishaji wa miundombinu ya usafari na usafirishaji, huduma za afya, elimu, maji, umeme, mawasiliano, michezo bila ya kuwaacha nyuma kinamama na vijana kwa kuwawezesha ili waweze kuinua vipato vyao. Tunamuunga mkono kwa nia yake thabit ya kuilinda na kuitunza miundombinu hiyo na rasilimali nyengine za nchi kwa manufaa ya wananchi wote na vizazi vijavyo. Mafanikio haya ni juhudi zake za kuleta

mageuzi ya kiuchumi na kijamii katika kuinua hali za wananchi wa Zanzibar. Kwa dhati nampongeza kwa **kuteuliwa kuendelea kupeperusha bendera ya Chama cha Mapinduzi kwa kugombea nafasi ya Urais wa Zanzibar**. Tunamuombea awe na afya njema na ushindi wa kishindo ili aendelee kuwatumikia na kukamilisha malengo makubwa aliyonayo kwa wananchi wa Zanzibar.

**6.0** **Mheshimiwa Spika,** Takriban miaka mitano sasa ya kukamilisha kipindi cha mwanzo cha Awamu ya Nane (8), Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameliongoza Taifa letu kwa umahiri na manufaa makubwa tumeyaona. Tumeshuhudia maendeleo katika nyanja zote za kiuchumi, ustawi wa jamii, Sheria, Umoja, Ushirikiano na Mshikamano baina ya wananchi wenyewe. Ahadi alizozitoa amezitimiza kwa kiwango cha juu.

**7.0** **Mheshimiwa Spika,** Naomba pia nitoe pongezi za dhati kwa **Makamo wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Masoud Othman** na Makamo wa Pili wa Rais **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla** wakiwa wasaidizi wakuu wa Mheshimiwa Rais. Juhudi zao zinasaidia kukuza na kuimarisha ustawi wa nchi na wananchi kwa ujumla. Nichukue fursa hii pia kumpongeza Katibu wa **Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said** kwa kusimamia Utumishi wa Umma na kutoa miongozo kupitia Kamati ya Makatibu Wakuu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu wote kwa ujumla awape umri na afya njema waendelee kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

**8.0** **Mheshimiwa Spika,** Kipekee, napenda kumpongeza **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa umahiri wake katika kuongoza ambao unatambuliwa na kuthaminiwa ndani na nje ya Tanzania, ukomavu wake wa kisiasa, kidemokrasia unaharakisha kufikia maendeleo yenye ufanisi mkubwa nchini Tanzania. Vile vile, tunampongeza

kwa kuteuliwa kuwa **Mgombea wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kupitia Chama cha Mapinduzi pamoja na **Dkt. Emmanuel John Nchimbi** kuteuliwa kuwa **Mgombea Mweza** katika uchaguzi ujao wa mwezi wa Oktoba 2025 kwa pamoja tunawaombea afya na ushindi mkubwa.

**9.0** **Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati naomba **nikushukuru wewe Spika wa Baraza la Wawakilishi Mheshimiwa Zubeir Ali** Maulid na Wasaidizi wako wote wakiwemo **Mheshimiwa Naibu Spika, na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu** za Baraza la Wawakilishi kwa ushirikiano wenu Baraza lako limekuwa ni sehemu ya mafanikio katika upangaji, utekelezaji na ufuatiliaji wa Mipango yetu. Hakika mnatusaidia sana Serikalini, ushauri na miongozo yenu imetuwezesha kuweza kufikia matarajio ya wananchi ya kuwaletea maendeleo na kuinua hali zao kimaisha na ustawi wao kiujumla.

**10.0** **Mheshimiwa Spika,** Tunafahamu ya kwamba mwaka 2025 ni **Mwaka wa Uchaguzi Mkuu nchini.** Viongozi kadhaa watachaguliwa moja kwa moja na wananchi kwa njia ya kura na wengine kuteuliwa kwa mujibu wa Katiba na Sheria. Tunawaombea kila la kheri wale wanaomaliza muda wao wa kulitumikia Taifa na Baraza lako tukufu na pia kuwatakia mafanikio wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watakaochaguliwa tena kuwatumikia wananchi kwa kutimiza ahadi zao kama watakavyozitoa wakati wa Kampeni. Kwa **Rais wetu Mpendwa** ambae kwa wananchi wengi wa Zanzibar, ameonekana kutokuwa na mbadala wake katika uchaguzi huo tunamuombea kila la kheri, afya njema na furaha katika maisha yake na familia yake kwa kuendelea kuwatumikia wananchi, kuwaletea maendeleo, kuimarisha umoja, amani na utulivu wa Taifa letu.

**11.0** **Mheshimiwa Spika,** Nitumie nafasi hii kutoa pole kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kufuatilia kifo cha **Bw. Charles Martin Hilary aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Mawasiliano Ikulu na Msemaji Mkuu wa Serikali**,

kilichotokea tarehe 14.05.2025. Marehemu Charles Hillary atakumbukwa milele katika tasnia ya habari kwa utendaji kazi mahiri, ucheshi, na ubunifu. Aidha, napenda kutoa pole kwako na kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi wote kwa ujumla kwa msiba uliolipata Baraza kufuatia kifo cha **Mheshimiwa Panya Ali Abdalla** aliyekuwa Mwakilishi wa Viti Maalum kilichotokea tarehe 26 Julai, 2024 alipokuwa akipatiwa matibabu nchini India katika kipindi ambacho tulikuwa tumeanza utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2024. Marehemu Bi. Panya atakumbukwa kwa mchango wake katika Baraza la Wawakilishi ikiwemo mchango wake alioukuwa akiutoa katika kuhakikisha utekelezaji wa umakini wa Mpango wa Maendeleo. Aidha, tunawaombea marehemu wote mapumziko mema. Pia, natuma salamu za pole ziwaendee wote walikumbwa na misiba ya kuondokewa na wana familia, jamaa, marafiki na watu wao wa karibu. ***Tunamuomba Mwenyezi Mungu awalaze marehemu wote mahala pema peponi, Amin!***

**12.0** **Mheshimiwa Spika,** sasa naomba kuwasilisha kwa muhtasari Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2024, Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 pamoja na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2025/2026.

## B. MAPITIO YA HALI YA UCHUMI 2024

**13.0** **Mheshimiwa Spika,** Mapitio haya yametokana na uchambuzi wa Viashiria vya uchumi jumuishi ambavyo ni muhimu katika kupanga maendeleo ya Taifa. Uchambuzi wa viashiria vya uchumi vimeweka misingi imara ya kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2025/26. Viashiria vilivyofanyiwa mapitio ni pamoja na: Pato la Taifa; Mfumuko wa bei; mwenendo wa Sekta ya nje; Sekta ya fedha; Deni la Serikali; na viashiria vya maendeleo ya watu ikiwemo idadi ya watu na hali ya umaskini nchini.

### *Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Dunia*

**14.0** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa taarifa ya Mtazamo wa Uchumi Duniani (World Economic Outlook,) iliyotelewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Mwaka 2025, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia katika mwaka 2024, imefikia wastani wa asilimia 3.2 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2023. Ukuaji huo umetokana na kuimarika kwa masoko ya fedha na mitaji duniani ambayo imepelekea kupungua kwa viwango vya gharama za riba za mikopo, kuongezeka kwa riba za uwekezaji na kuimarika kwa miundombinu ya usafirishaji wa bidhaa duniani. Hata hivyo, bado ukuaji huu wa uchumi ni wa chini ukilinganisha na ukuaji wa uchumi wa wastani wa asilimia 3.8 kabla ya mripuko wa ugonjwa wa COVID-19.

**Hali ya Ukuaji wa Uchumi duniani ni kama ifuatavyo:-**

i. **Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Zilizoendelea (Developed Economies)** umefikia wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 1.6 kwa mwaka 2023 ukuaji huo umetokana na kuongezeka kwa biashara za Kimataifa na kuongezeka kwa thamani ya uwekezaji katika masoko ya mitaji.

ii. **Kwa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibuka Kiuchumi (Developing and Emerging Economies)** ukuaji wa uchumi umefikia wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2024, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2023. Ukuaji huo umetokana na kuongezeka kwa thamani ya masoko ya fedha na mitaji na kukua kwa biashara za usafirishaji wa bidhaa za viwandani zenye umiliki na uwakala kutoka katika kampuni za Marekani na Ulaya.

iii. **Uchumi wa Nchi za Afrika**, kasi ya ukuaji wa uchumi imefikia wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2023. Ukuaji huo umetokana na kuongezeka kwa matumizi ya huduma za nishati ya umeme na gesi na kuongezeka kwa uzalishaji wa mafuta kwa nchi wazalishaji wakubwa wa mafuta katika Bara hili zikiwemo **Libya** asilimia 7.6, **Angola** asilimia 4.4, **Algeria** asilimia 3.6 na **Nigeria** asilimia 3.4.

iv. **Kwa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara (Sub Saharan Countries)**, kasi ya ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2024 imefikia wastani wa asilimia 3.8 kutoka wastani wa asilimia 3.6 mwaka 2023. Hii imetokana na utekelezaji wa sera za udhibiti wa matumizi ya fedha za kigeni sambamba na sarafu za nchi hasa Dola ya Marekani kulikopelekea kuimarika kwa sarafu zao pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji viwandani. Nchi zilizokuwa kwa kasi zaidi katika ukanda huu ni pamoja na **Benin** ukuaji wa asilimia 7.5, **Bukina Faso** asilimia 4.1, **Niger** asilimia 10.4, **Afrika ya Kati** (Central Africa) asilimia 3.8 na **Senegal** asilimia 9.3.

v. **Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki,** kasi ya ukuaji uchumi imefikia wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2023. Ukuaji huu umetokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mafuta na usafirishaji. Hali hii ni baada ya kurejea kwa udhibiti wa miundombinu ya kusafirishia mafuta nchini Sudan ya Kusini, kuongezeka kwa thamani ya usafirishaji wa mazao na bidhaa za viwandani, kuongezeka kwa mitaji ya uwekezaji na kuimarika kwa masoko ya hisa. Katika Afrika Mashariki, nchi zilizokuwa zaidi ni pamoja na **Uganda** asilimia 6, **Tanzania** asilimia 5.4 na **Burundi** asilimia 4.6.

**Hali ya Mfumuko wa Bei Duniani**

**15.0 Mheshimiwa Spika,** Ufuatiliaji wa mwenendo wa kasi ya mfumuko wa bei duniani ni muhimu sana katika kubuni sera na mikakati ya kudhibiti athari za kupanda kwa bei za bidhaa zinazoagizwa kutoka nje. Kama tunavyofahamu kupungua kwa kasi ya mfumuko wa bei za bidhaa na huduma huongeza thamani na kupunguza nguvu ya usawa katika ununuzi. Wastani wa kasi ya mfumuko wa bei duniani imefikia asilimia 5.8 kutoka asilimia 6.8 mwaka 2023. Hii imetokana na kupungua kwa bei za bidhaa, viwango vya riba na udhibiti wa sera za kifedha, ikiwemo kupunguza matumizi ya Dola ya Marekani kama sarafu kuu kwa uhaulishaji wa biashara za Kimataifa baina ya nchi wanachama

wa nchi za BRICS. Mfumko wa bei una sura tafauti kwa maeneo mengine duniani kama ifuatavyo:

i. Kasi ya mfumko wa bei kwa **Nchi Zilizoendelea** imepunguwa kwa wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2023 kutokana na utekelezaji wa sera ya kupunguza matumizi ya dola ya Marekani kama sarafu ya kuhaulisha bidhaa baina ya Washirika wa biashara za Kimataifa.

ii. **Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi** zimefikia wastani wa asilimia 7.9 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 8.1 mwaka 2023. Kupungua kwa mfumuko wa bei kumetokana na utulivu wa bei za mafuta na kupungua kwa bei za chakula na bidhaa za viwandani.

iii. Kasi ya mfumko wa bei katika ukanda wa **Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara** imeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 18.1 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 17.6 mwaka 2023. Ongezeko hili limesababishwa na kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya chakula kutokana na athari za mabadiliko ya tabia nchi kama vile ukame na mafuriko katika nchi za Malawi, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Chad. Sababu nyengine ni pamoja na kuendelea kwa machafuko ya kisiasa nchini Ethiopia na vita katika nchi za Sudan na Jamhuri ya Demokrasia ya Congo.

iv. Kasi ya Mfumko wa bei kwa **Jumuiya ya Afrika Mashariki** imepungua na kufikia wastani wa asilimia 10.5 mwaka 2024, kutoka wastani wa asilimia 11.6 mwaka 2023. Hii imesababishwa na kupungua kwa gharama za uagiziaji wa bidhaa kutokana na kuimarika kwa miundombinu ya usafiri na ufanisi wa bandari tegemezi hasa kwa nchi za Tanzania na Kenya.

## Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Zanzibar

**16.0** **Mheshimiwa Spika,** Juhudi za dhati za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kipindi hichi cha Serikali

ya Awamu ya Nane (8) za kuleta **Mapinduzi ya kiuchumi na kuimarisha hali za wananchi** na utoaji wa huduma zinaonekana wazi wazi. Kwa mujibu wa viashiria vya kiuchumi, Pato Halisi la Taifa (GDP at constant prices) limeongezeka na kufikia thamani ya **TZS 4,026.4 bilioni** mwaka 2024 kutoka thamani ya **TZS 3,758.6** bilioni mwaka 2023 sawa na kasi ya ukuaji wa asilimia 7.1 kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia **7.4** mwaka 2023. Pato la Taifa kwa bei ya soko (GDP at current price) limeongezeka na kufikia thamani ya **TZS 6,572.6 bilioni** mwaka 2024 kutoka thamani ya **TZS 6,041.3 bilion**i mwaka 2023. Miongoni mwa sababu za ukuaji wa uchumi kwa asilimia **7.1** ni pamoja na:

i. Kuimarika kwa Sekta ya Kilimo, katika Sekta ndogo ya Mazao kufikia ukuaji wa asilimia 6.4 mwaka 2024 kutoka ukuaji wa asilimia 2.8 mwaka 2023;
ii. Kukua kwa Sekta ya Uvuvi kufikia asilimia 14.2 kutoka asilimia 8.1 mwaka 2023;
iii. Kuongezeka kwa watalii waliotembelea Zanzibar kufikia watalii 736,755 mwaka 2024 kutoka watalii 638,498 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 15.4;
iv. Kuongezeka kwa miradi mipya ya uwekezaji kwa asilimia 13.0 kufikia miradi 131 yenye thamani ya **TZS 1,887.7 bilioni** iliyosajiliwa mwaka 2024 kutoka miradi 114 iliyosajiliwa mwaka 2023;
v. Kuongezeka kwa shughuli za Uchimbaji Mawe na Mchanga kwa ajili ya sekta ya ujenzi kwa asilimia 17.0 mwaka 2024 kutoka asilimia 10.4 mwaka 2023;
vi. Kuongezeka kwa mapato ya ndani kufikia **TZS 1,279.0** bilioni mwaka 2024/25 sawa na asilimia 97.1 ya makadirio ya kipindi hicho ikilinganishwa na jumla ya **TZS 1,075.9 bilioni** zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/2024.

**17.0 Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa sababu zilizopelekea kushuka kidogo kwa kasi ya ukuaji wa uchumi mwaka 2024 ikilinganishwa na mwaka 2023 kumetokana na kupungua kwa kasi ya ukuaji kwa baadhi ya sekta ikiwemo:

i. Sekta ya ndogo ya uzalishaji viwandani kutoka wastani wa asilimia 6.9 mwaka 2023 kufikia wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2024 kutokana na kupungua kwa uzalishaji wa sukari kutoka kiwanda cha Sukari Mahonda.
ii. Sekta ndogo ya misitu imepungua kutoka wastani wa asilimia 6.4 kufikia wastani wa asilimia 0.1 mwaka 2024. Hii ni kutokana na kuhamasika kwa jamii kutumia nishati mbadala ya kupikia hususani gesi na kupungua kwa matumizi ya mkaa na kuni pamoja na na kusimamia Mkakati wa Serikali wa Kupunguza Ukataji wa Miti kwa ajili ya mkaa;
iii. Sekta ndogo ya fedha (huduma za kibenki) imepungua kutoka wastani wa asilimia 54.6 mwaka 2023 kufikia wastani wa asilimia 13.7 mwaka 2024 kutokana na kupungua kwa mitaji ya akiba za kibenki .

**Pato la Mwananchi**

**18.0 Mheshimiwa Spika,** Kuongezeka kwa Pato la Taifa kumepelekea kuongezeka kwa kipato cha mwananchi mmoja mmoja. Kwa mwaka 2024, Pato la Mwananchi Zanzibar limeongezeka na kufikia TZS 3.2 milioni sawa na Dola za Kimarekani 1,395 kutoka TZS 3.1 milioni sawa na Dola za Kimarekani 1,241 mwaka 2023. Zanzibar inakadiriwa kufikia idadi ya watu 2.036 milioni mwaka 2024 ambapo kasi ya ongezeko la idadi ya watu limefikia wastani wa asilimia 3.7.

**Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Zanzibar**

**19.0 Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2024, Kasi ya mfumuko wa bei imepunguwa na kufikia wastani wa asilimia 5.1 kutoka wastani wa asilimia 6.9 mwaka 2023. Kupungua huko kumetokana na kupungua kwa mfumuko wa bei wa bidhaa za chakula na zisizo za chakula katika soko. Kwa mwaka 2024, bidhaa za chakula zimepungua na kufikia wastani wa asilimia 8.4 kutoka wastani wa asilimia 11.1 mwaka 2023, na bidhaa zisizo za chakula zimefikia wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2023.

**20.0 Mheshimiwa Spika,** Kasi ya mfumuko wa bei Zanzibar ingeweza kuwa ya juu zaidi lakini Serikali inaendelea kuchukua hatua za kupunguza na kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha upatikanaji wa huduma na bidhaa muhimu kwa wananchi. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuendelea kutoa bei elekezi na kusimamia bidhaa zinazoingia nchini zikiwemo bidhaa za chakula na vifaa vya ujenzi, kupitia **Benki Kuu ya Tanzania (BoT)** inaendelea kufuatilia na kuchukua hatua za kudhibiti sera za kifedha ikiwemo kushuka kwa thamani kwa sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine duniani.

**HALI YA AJIRA**

**21.0 Mheshimiwa Spika,** Kuimarika kwa shughuli za uzalishaji wa ndani pamoja na hali ya amani na utulivu kumeongeza ajira rasmi na zisizo rasmi. Kwa mwaka 2023/2024, jumla ya ajira mpya zilizosajiliwa kutoka Serikalini, Mashirika ya Serikali na Sekta Binafsi zimefikia ajira 83,430 (wanaume ni 43,629 na wanawake ni 39,801) ikilinganishwa na ajira 82,225 (wanaume ni 43,643 na wanawake ni 38,582) ambazo zilisajiliwa mwaka 2022/2023. Ajira zilizotolewa na Sekta binafsi katika kipindi hichi zimefikia 36,716 na za Sekta za Umma ni 46,714. Kuongezeka kwa ajira mpya mwaka 2023/2024 kumetokana na kuongezeka kwa uhitaji wa wafanyakazi katika sekta ya Elimu ambayo imeajiri wafanyakazi 25,017 ikifuatiwa na Sekta ya Utawala wa Umma ajira mpya 11,726. Sekta binafsi imeendelea kuwa na mchango mkubwa katika kuongeza uzalishaji wa ndani, upatikanaji wa ajira, ukusanyaji wa mapato, uingizaji wa fedha za kigeni, uimarishaji wa miundombinu na kukuza hali za uchumi kwa wananchi. Kupitia Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kwa mwaka 2024 miradi mipya iliyotoa ajira nyingi zaidi kuliko miradi mengine ni miradi ya hoteli na migahawa kufikia ajira mpya 1,834, ikifuatiwa na miradi ya uwekezaji wa nyumba za biashara (Real Estate) kufikia ajira mpya 933, na miradi ya kilimo, misitu na uvuvi kufikia ajira mpya 454.

22.0 **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na ajira hizo, mwaka 2024/2025 Serikali pia imeweza kuratibu ajira 5,830 (Wanawake 5,015 na Wanaume 815) za Nje ya Nchi ikilinganishwa na ajira 3,780 kwa mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 54.2. Takwimu zinaoonesha kuwa **vijana wa Kizanzibari wameajiriwa kwa kazi zisizo za kitaalamu katika nchi za Qatar, Oman, Kuweiti, Saudi Arabia na UAE,** waajiriwa hao wameajiriwa katika kazi za vibarua, udereva, mahotelini na kazi za majumbani. Juhudi za kuwaendeleza kielimu Wazanzibari zinaendelea ili waweze kupata ajira zenye tija zaidi.

## MWENENDO WA THAMANI YA SHILINGI YA TANZANIA DHIDI YA DOLA YA MAREKANI

23.0 **Mheshimiwa Spika,** Mwenendo wa thamani ya sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine Duniani ni muhimu kutokana na mauzo na ununuzi wa bidhaa nje ya nchi. Kwa mwaka 2024, Shilingi ya Tanzania imeshuka thamani dhidi ya Dola ya Kimarekani kufikia thamani ya TZS 2,603.11 kwa Dola moja ikilinganishwa na wastani wa thamani ya TZS 2,506.0 kwa Dola moja kwa mwaka 2023. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya fedha za kigeni nchini. Hata hivyo, Shilingi ya Tanzania mwaka 2024 imeshuka thamani kwa wastani wa asilimia 3.8 ikilinganishwa na mwaka 2023 ilishuka thamani kwa wastani wa asilimia 8.4. **Benki Kuu ya Tanzania** inaendelea kuchukua hatua za kudhibiti kushuka kwa thamani Sarafu ya Tanzania na kuongeza mzunguko wa Fedha (money circulation), kupitia kuimarisha sera za fedha pamoja na uuzaji na usafirishaji wa Madini yakiwemo dhahabu. Serikali inaendelea na kuimarisha na kushajihisha uzalishaji wa mazao ya biashara na kuimarisha vivutio vya utalii ili kuwa na akiba ya kutosha ya fedha za kigeni.

24.0 **Mheshimiwa Spika,** fedha za kigeni zinaendelea kuhifadhiwa (Foreign reserve) ili kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Katika kipindi cha mwaka 2023/24, kiwango cha akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani 5.3

bilioni ikilinganishwa na dola za Marekani 5.2 bilioni kipindi kama hicho mwaka 2022/2023. Kiasi hicho kinatosheleza malipo ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 4.4. Kiasi hicho ni zaidi ya lengo la nchi la kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayokidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi isiyopungua minne.

**SEKTA YA UTALII**

25.0 **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea na kuimarisha sekta ya utalii ikiwa ni kiongozi kwa uchumi wa Zanzibar inayochangia karibu asilimia 30 ya Pato la Taifa. Mwaka 2024, idadi ya watalii waliotembelea Zanzibar kupitia kiwanja cha ndege na bandari ya Zanzibar imeongezeka kwa asilimia 15.4 na kufikia watalii 736,755 kutoka watalii 638,498 mwaka 2023. Ongezeko hilo limepelekea kuongezeka kwa thamani ya mauzo yatokanayo na uhaulishaji wa huduma (Receipts from Service Account) yenye Dola za Kimarekani 1,046.5 milioni kwa mwaka ulioishia Disemba 2024, kutoka Dola za Kimarekani 906 milioni mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 15.4. Jitihada zilizochukuliwa na Serikali kuimarisha sekta ya utalii ni pamoja na:

i. Kuitangaza Zanzibar Kimataifa na ziara za Viongozi Wakuu, Mawakala wa usafirishaji watalii pamoja na Mabalozi wetu wa Tanzania nje ya nchi kupitia maonyesho na makongamano;
ii. Kuendelea kushajihisha uwekezaji wa miradi mikubwa ya hoteli za nyota tano;
iii. Kuhamasisha masoko mapya ya utalii na kuleta ndege za moja kwa moja (Direct Flights) kuja Zanzibar;
iv. Kutangaza utalii wa ndani kwa kuanzisha programu mbalimbali za kuonesha vivutio vya ndani na kushiriki maonesho ya Kimataifa na ya kikanda, matamasha, kongamano na warsha;
v. Kuendelea kuimarika kwa hali ya amani na utulivu nchini.

**26.0** **Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa nchi ambazo zimeongoza kwa kuleta watalii wengi mwaka 2024 ni Ulaya kwa watalii 92,449 sawa (ongezeko la asilimia 12.5), **Italia** watalii 87,202 sawa (ongezeko la wastani wa asilimia 11.8), **Ujerumani** watalii 71,283 sawa (ongezeko la asilimia 9.7), **Ufaransa** watalii 69,557 sawa (ongezeko la asilimia 9.4), **Uingereza** watalii 42,244 sawa (ongezeko la asilimia 5.7) na nchi nyengine za **Afrika** watalii 40,475 sawa (ongezeko la asilimia 5.5).

## SEKTA YA NJE

### Urari wa Biashara

**27.0** **Mheshimiwa Spika,** Nakisi ya biashara kwa mwaka imeongezeka kufikia thamani ya TZS 1.5 trilioni kutoka thamani ya TZS 1.3 trilioni mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 10.8, hali hii ni kutokana na kuongezeka kwa uagiziaji wa bidhaa kutoka nje kuliko usafirishaji. Thamani ya **Uagiziaji** wa bidhaa kutoka nje ya nchi imefikia TZS 1.6 trilioni mwaka 2024 kutoka thamani ya TZS 1.5 trilioni mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 9.8. Bidhaa zilizoingia nchini ni mashine, vifaa vya viwandani na zana za kilimo (Capital goods) zenye thamani ya TZS 377.9 bilioni; bidhaa za nishati ya mafuta na mali ghafi za viwandani (Intermediate goods) zenye thamani ya TZS 871.2 bilioni na bidhaa za matumizi ya kila siku kama vyakula, nguo (Consumer goods) zenye thamani ya TZS 400.0 bilioni.

**28.0** **Mheshimiwa Spika,** Usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya nchi umefikia thamani ya TZS 105.2 bilioni kutoka thamani ya TZS 109.2 bilioni ya mwaka 2023 sawa na upungufu wa asilimia 3.6. Bidhaa zilizotoka Zanzibar zimesafirishwa katika nchi za India, Singapore, Uganda, Oman na Umoja wa Falme za Kiarabu (U.A.E). Mazao ya biashara yanayosafirishwa kutoka Zanzibar ni zao la karafuu na mwani, mazao mengine ni majongoo bahari (sea cucumbers), viungo (spices) na dagaa. Usafirishaji wa zao la karafuu umefikia jumla ya tani 1,974.4 zenye thamani ya TZS 30.7 bilioni kutoka tani 3,197.3 zenye thamani ya TZS 47.0 bilioni

zilizosafirishwa mwaka 2023, sawa na upungufu wa thamani kwa asilimia 34.7.

**29.0** **Mheshimiwa Spika,** Kupungua kwa usafirishaji wa zao la karafuu kumetokana na msimu mdogo wa zao hilo. Usafirishaji wa zao la mwani umefikia tani 7,089.5 zenye thamani ya TZS 10.7 bilioni kutoka tani 11,737.3 zenye thamani ya TZS 19.2 bilioni zilizosafirishwa mwaka 2023. Kupungua kwa usafirishaji wa zao la mwani ni kutokana na kushuka kwa thamani ya sarafu ya Dola ya Kimarekani mwaka 2024 jambo lililosababisha baadhi ya Makampuni kupunguza usafirishaji wa mwani kwa kiwango kikubwa kuepuka hasara inayoweza kutokea katika biashara hiyo na ushindani mkubwa wa uzalishaji wa zao la mwani kwa baadhi ya nchi kama Indonesia na China.

**Mwenendo wa Biashara Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara (Intra trade)**

**30.0** **Mheshimiwa Spika,** Uhaulishaji wa bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara kwa mwaka 2024 umeongezeka kufikia thamani ya TZS 280.8 bilioni kutoka thamani ya TZS 159.7 bilioni mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 75.8. Bidhaa zilizohaulishwa ni mafuta ya kula na chuma chakavu. Aidha, uhaulishaji wa bidhaa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar umeongezeka kufikia thamani ya TZS 549.6 bilioni mwaka 2024 kutoka thamani ya TZS 431.5 bilioni mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 27.3. Bidhaa zinazohaulishwa zaidi ni bidhaa za chakula ikiwemo mchele wa mbeya, mboga mboga na unga wa mahindi.

**Ukuzaji Rasilimali**

**31.0** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2024, Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) imesajili miradi 131 yenye thamani ya TZS 1.8 trilioni kutoka miradi 114 yenye thamani ya TZS 4.6 trilioni mwaka 2023 sawa na asilimia hasi 59.5 ya thamani ya

miradi hiyo. Kupungua kwa thamani ya miradi hiyo kumetokana na kupungua kwa thamani ya miradi iliyowekezwa mwaka 2024. Miradi yenye thamani kubwa zaidi iliyowekezwa nchini ni miradi ya nyumba za biashara/mali zisizohamishika (Real Estate) yenye thamani ya TZS 902.6 bilioni ikifuatiwa na miradi ya hoteli na migahawa (Accommodation and Food Services) yenye thamani ya TZS 553.1 bilioni.

**Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

**32.0** **Mheshimiwa Spika,** Wanafunzi waliopata mikopo ya elimu juu kwa Mwaka 2024/25 wameongezeka kufikia wanafunzi 4,629 kutoka 2,502 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 85.0. Hii imetokana na kuongezeka kwa ufaulu kwa kuwa na wanafunzi wengi wenye sifa ya kuendelea na masomo ya elimu ya juu katika ngazi tofauti ikiwemo ngazi ya Diploma. Serikali pia imeongeza fungu la mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka TZS 29.0 bilioni mwaka 2023/24 kufikia TZS 30.5 bilioni mwaka 2024/25 sawa na ongezeko la asilimia 5.2. Vile vile, hadi kufikia Machi 2025, TZS 3.4 bilioni zilikusanywa kama marejesho ya mikopo ya elimu ya juu sawa na asilimia 82.0 ya lengo la mwaka, kutoka TZS 3.1 bilioni mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 9.6.

**Uanzishwaji wa Zanzibar SUKUK**

**33.0** **Mheshimiwa Spika,** Katika mafanikio ya kihistoria, tarehe 22 Februari 2025, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilizindua Sukuk ya Kwanza ya Quasi-Sovereign SUKUK ya Zanzibar yenye thamani ya TZS trilioni 1.115 (takribani USD milioni 414), ikiwa ni Sukuk ya kwanza kutolewa na Serikali katika Afrika Mashariki na Kati. Sukuk ni utaratibu wa uwekezaji wa fedha kwa mfumo wa Hati Fungani Unaozingatia Misingi ya Shariah, uliopangwa kwa mujibu wa Mkataba wa “Manfa’a Ijarah”. Sukuk ya Zanzibar inatarajiwa kuiva mwaka 2032. Awamu ya kwanza ilikuwa na thamani ya TZS bilioni 300 ambapo wawekezaji waliwekeza zaidi ya TZS 381 bilioni (takribani USD milioni 111), ambayo inatoa

fursa ya uwekezaji kwa kutumia Shilingi za Kitanzania au Dola za Kimarekani, huku ikitoa viwango vya faida ya kila mwaka vya asilimia 10.5 (TZS) na asilimia 4.2 (USD). Utoaji wa Sukuk ya Zanzibar ni hatua kubwa kwa maendeleo ya sekta ya fedha ya Kiislamu nchini Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla. Nichukue fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza wajumbe wa Baraza hili na Watanzania waliowekeza katika Zanzibar Sukuk na kumuunga mkono Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kuharakisha maendeleo ya Zanzibar.

**34.0** **Mheshimiwa Spika,** Sukuk ya Zanzibar inatarajiwa kuwavutia wawekezaji mbali mbali ikiwa ni pamoja na mabenki ya Kiislamu, wawekezaji wa taasisi na watu binafsi, wana diaspora na hata wageni wanaomiliki akaunti za benki ndani ya Tanzania sambamba na kutoa fursa kwa wananchi kushiriki moja kwa moja katika ujenzi wa Taifa huku ikipunguza utegemezi wa mikopo ya kigeni yenye riba kubwa. Sukuk ina mvuto maalum kwa wawekezaji wanaotaka kuwekeza katika njia halali kulingana na Shariah, na hivyo kuongeza fursa chache zilizokuwepo awali. Hatua hii itasaidia kuimarisha masoko ya mitaji ya Tanzania na kuhamasisha ushiriki wa wawekezaji wa nje.

## c. UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI 2024 – MACHI 2025)

**35.0** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2024/2025 **Mpango wa Maendeleo** ulipangwa kutumia kiasi cha TZS 3,271.11 bilioni sawa na asilimia 63.11 ya Bajeti ya Serikali kwa kutekeleza Programu na Miradi ya Maendeleo (TZS 3,263.07 bilioni kwa Miradi ya Serikali Kuu na TZS 8.03 bilioni kwa miradi ya Serikali za Mitaa). Kati ya fedha hizo Programu na Miradi ya Kimkakati imepangiwa kutumia jumla ya TZS 2,086.72 bilioni (TZS 1,049.58 bilioni kutoka Serikalini na TZS 1,005.13 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

**36.0** **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miezi tisa Julai 2024 hadi Machi 2025, programu na miradi **20** imetekelezwa sawa na ongezeko la asilimia **43** ikilinganishwa na programu na miradi 14 iliotekelezwa katika kipindi kama hiki 2023. Hadi kufikia Machi 2025, TZS 691.62 bilioni sawa na asilimia 61 ya lengo la 1,130.1 bilioni zimepatikana (TZS 508.7 bilioni kutoka Serikalini sawa na asilimia 88 ya lengo na TZS 182.9 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 33 ya lengo).

**Utekelezaji wa Maeneo ya Kimkakati kwa Kipindi cha Miezi Tisa (Julai 2024 -Machi 2025)**

**37.0** **Mheshimiwa Spika,** Serikali imegharamia utekelezaji wa miradi ya kimkakati kupitia **Maeneo Makuu Matano (5)** ambayo ni: Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu; Mazingira Wezeshi na Kuimarisha Miundombinu; Kuimarisha Mageuzi ya kiuchumi; Kukuza Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii; pamoja na Kuimarisha Utawala Bora na Uhimilivu kama yalivyoanishwa katika Mpango wa Maendeleo (ZADEP) 2021-2026. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Programu na Miradi ya Kimkakati imepangiwa kutumia jumla ya TZS 1,130.1 bilioni (TZS 577.3 bilioni kutoka Serikalini na TZS 552.8 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 691.62 bilioni sawa na asilimia 61 ya lengo la 1,130.1 bilioni zimepatikana (TZS 508.7 bilioni kutoka Serikalini sawa na asilimia 88 ya lengo na TZS 182.9 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 33 ya lengo). Utekelezaji wa Programu na Miradi hiyo kwa maeneo ni kama ifuatavyo:-

**I. Kutumia fursa za Uchumi wa Buluu**

**38.0** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2024/2025, eneo hili lilipangiwa kutekeleza programu moja (1) na miradi minne (4) ya maendeleo ambayo imepangiwa kugharimu kiasi cha TZS 453 bilioni. Kwa kipindi cha miezi tisa Julai 2024 hadi Machi 2025, programu na miradi hiyo ilipangiwa kiasi cha TZS 256.5 bilioni. Hadi kufikia

Machi 2025, TZS 163.2 bilioni sawa na asilimia 64 ya lengo la TZS 256.5 bilioni zimepatikana. Utekelezaji wa eneo hili ni kama ifuatavyo: -

**a)** ***Programu ya Uimarishaji wa Maeneo ya Kihistoria katika Maeneo ya Fukwe:*** Programu ina lengo la kuendeleza Sekta ya Utalii kwa kuimarisha na kuyahifadhi maeneo ya kihistoria na kukuza utalii ambao utaongeza fursa za ajira, vivutio na Pato la Taifa. Hadi kufikia Machi 2025, Eneo la Mangapwani limeimarishwa kwa kujenga ukuta wa kuzuia athari za bahari pamoja na kuweka ardhi sawa. Kufanya Matengenezo jengo la Ngome Kongwe kwa kuliwekea theatre na kuliweka katika mazingira mazuri ,ujenzi umefikia asilimia 74. Katika uimarishaji wa maeneo ya kihistoria pia Ras Mkumbuu ukarabati wa majengo umefikia asilimia 77 ya utekelezaji.

**b)** ***Mradi wa Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki:*** Mradi huu una lengo la kuwawezesha wavuvi kupata huduma za msingi za bandari na masoko kwa kuwajengea madiko na masoko ya kuhifadhia na kuuzia samaki yenye hadhi ya kisasa katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi 2025, Ujenzi wa ukuta wa kuzungusha eneo lisiathiriwe na maji ya chumvi, ujenzi wa daraja kwa ajili ya kupita wananchi na kingo za maji umekamilika kwa Mkoani Pemba, kazi zinazoendelea ni Ujenzi wa jengo la biashara na ofisi ambapo upo katika hatua ya kuweka zege kwa ajili ya ghorofa ya pili. Aidha, ujenzi wa miundombinu ya barabara za ndani unaendelea. Kwa upande wa Unguja hatua za maandalizi ya ujenzi wa soko la kisasa la Samaki katika eneo la Fungurefu zinaendelea baada ya Mkandarasi kukabidhiwa eneo kwa ajili ya ujenzi.

**c)** ***Mradi wa Ujenzi wa Bandari Jumuishi – Mangapwani:*** Mradi huu ni wa ujenzi wa bandari jumuishi (Multipurpose

Port) katika eneo la Mangapwani ambayo inajumuisha ujenzi wa gati ya mizigo eneo la ushushaji na upakiaji wa mafuta na chelezo cha kukarabati meli. Hadi kufikia Machi 2025, ujenzi wa nyumba za fidia na miundombinu ya barabara, umeme na maji kwa ajili ya uwekezaji wa bandari hiyo unaendelea. Jumla ya kilomita 5.8 zimeshawekwa lami na kilomita 6.2 zinaendelea. Kwa upande wa ujenzi wa bandari Awamu ya kwanza, Mkandarasi Kampuni ya CHECC ya nchini CHINA imekabidhiwa eneo la ujenzi na kazi za utafiti wa udongo na bahari zinaendelea.

d) ***Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Abiria Maruhubi:*** Mradi unahusisha ujenzi wa gati ya abiria na gati ya mizigo (RORO) katika eneo hilo. Hadi kufikia Machi 2025, kazi ya upimaji wa udongo imekamilika na Mkandarasi ameanza kuleta vifaa kwa ajili ya kuanza kazi. Aidha, kazi ya ufukiaji wa eneo la juu la bahari imeanza ili kuweka usawa wa eneo.

e) ***Mradi wa Ununuzi wa Boti mbili za Serikali:*** Mradi huu una lengo la kuimarisha usafirishaji wa abiria na mizigo kwa wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba ili kupunguza changamoto za usafiri zinazoikabili Zanzibar. Hadi kufikia Machi 2025, michoro imeandaliwa na kuwasilishwa kwa Kampuni ya RINA- Classification Society ya nchini Italy kwa ajili ya kuthibitishwa (Approval). Malipo ya awali yameshafanyika kwa Kampuni ya Synergy Shipbuilder ya India kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa boti. Mradi huu unatekelezwa na Shirika la Meli kwa mkopo wa Dola za Kimarekani USD 27 milioni kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) uliodhaminiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

### II. Mazingira Wezeshi na Kuimarisha Miundombinu

**39.0 Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2024/2025, eneo hili limepangiwa kutekeleza programu tatu (3) na miradi mitatu (3) ya

maendeleo ambayo itagharimu **TZS 811.10 bilioni.** Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **TZS 428.0 bilioni** zimepangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha **TZS 250.0 bilioni** sawa na asilimia 58 ya lengo la **TZS 428.0 bilioni** zimepatikana. Utekelezaji wa eneo hili ni kama ifuatavyo: -

**a)** ***Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu:*** Programu hii imeanza mwaka 2022/23 na ina lengo la kujenga barabara kwa kiwango cha lami, ujenzi wa mitaro pamoja na uwekaji wa taa na alama za barabarani Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi 2025, kazi ya uwekaji lami kwa barabara zenye urefu wa km 16 kati ya km 22.1 kwa barabara ya Wete – Chake Chake imekamilika, km 3.6 kutoka Mzambarauni hadi Weni zimeshawekwa kifusi katika matabaka mbali mbali. Kwa bara bara za Jozani-Charawe, Ukongoroni –Bwejuu km 23.3, Fuoni Tunguu km 5.8, barabara za Nungwi km 13.35 na barabara ya Bungi km 0.5 zimekamilika kwa asilimia 100.

**b)** ***Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani:*** Programu itahusisha ujenzi wa barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9 katika maeneo ya mijini na vijijini Unguja na Pemba. Kiasi cha km 59.93 za barabara zimeshawekwa lami na km 35.86 ziko katika hatua ya uwekaji wa kifusi kwa tabaka mbali mbali. Aidha, uwekaji wa alama za barabarani kwa baadhi ya barabara za ndani umeanza utekelezaji ni asilimia 30.

**c)** ***Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini:*** Programu ina lengo la kuweka haiba ya mji wa Zanzibar kwa ujenzi wa barabara zenye urefu wa km 100.9 katika maeneo ya mjini. Hadi kufikia Machi 2025, ujenzi wa barabara uko katika hatua mbali mbali ikiwemo uwekaji wa lami, zege, mitaro, alama na taa kwa barabara zinaendelea. Kwa upande wa barabara ya juu ya Mwanakwerekwe (Flyover) kazi inayoendelea kwa sasa ni ujenzi wa chelezo kwa

pande zote mbili za daraja na ujenzi umefikia asilimia 90 na ujenzi wa flyover ya Amani hatua iliofikia ni kunyanyua nguzo zitakazobeba *flyover.*

d) ***Mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege- Pemba:*** Mradi huu una lengo la kuimarisha miundombinu ya usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya anga ili iweze kuwa katika viwango vya Kimataifa. Hadi kufikia Machi 2025, Fidia imeshalipwa kwa wananchi 727 ili kupisha eneo la ujenzi wa Uwanja wa Ndege. Mkandarasi ameshaanza kazi za usambazaji wa vifaa na wataalamu pamoja na kukamilisha ujenzi wa maabara. Pia, Mkandarasi anaendelea na kazi za usanifu wa michoro ambapo tayari ameshawasilisha rasimu ya Ripoti ya awali (Inception report).

e) ***Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko sekta ya Nishati (ZESTA):*** Katika kuimarisha sekta ya umeme, mradi utahusisha usambazaji wa umeme katika maeneo tofauti ya visiwa vya Unguja na Pemba na usafishaji wa eneo kwa ajili ya umeme wa jua (Solar Panel). Mkandarasi amekamilisha kupima njia ya umeme, maeneo yote ya ujenzi wa vibanda vya umeme yameshatayarishwa pamoja na utoaji wa mafunzo kwa wataalamu wa Shirika la Umeme (ZECO).

f) ***Mradi wa Ujenzi wa Kituo na Maegesho ya Vyombo vya Usafiri Soko la Mwanakwerekwe:*** Mradi huu una lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi na wafanyabiashara kwa kujenga kituo cha maegesho ya vyombo vya usafiri na huduma nyengine za usafiri katika Soko la Mwanakwerekwe ili kuongeza ufanisi wa upatikanaji wa huduma za soko, kupunguza msongamano wa vyombo na kuongeza Pato la Taifa. Hadi kufikia Machi 2025, hatua za awali za utekelezaji zimeanza kwa kufanya Upembuzi Yakinifu ikiwemo utafiti wa Mazingira na kuangalia sayansi ya udongo na umbile la ardhi ya eneo husika (geotechnic survey and topographic) kazi hii inaendelea.

**Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi**

**40.0 Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2024/2025 eneo hili lilipangiwa kutekeleza programu moja (1) na miradi miwili (2) ya maendeleo ambayo imegharimu jumla ya TZS 65.3 bilioni. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024–Machi 2025) TZS 35.9 bilioni zimepangwa. Hadi kufikia Machi 2025, TZS 4.1 bilioni sawa na asilimia 11 ya lengo la TZS 35.9 bilioni zimepatikana. Utekelezaji wa eneo hili ni kama ifuatavyo:

a) ***Programu ya Uimarishaji wa Maeneo Huru ya Uwekezaji:*** Programu hii ina lengo la kukuza maeneo huru ya uwekezaji kwa kuimarisha miundombinu ya barabara, maji, umeme na mawasiliano katika maeneo yote yaliyoainishwa kwa uwekezaji ili kuwavutia Wawekezaji wa ndani na nje ya Zanzibar. Hadi kufikia Machi 2025, kazi ya ukamilishaji wa tathmini ya ulipaji fidia inaendelea na Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara ameshapatikana. Mikataba tayari imeshasainiwa baina ya Mamlaka ya Kukuza Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) kwa upande wa Serikali na Kampuni ya CRJE (East Africa) Ltd kwa ujenzi wa km 35 za barabara za Zone B Micheweni na Fumba, Zabuni kwa ajili ya upelekaji wa miundombinu ya barabara kwa eneo la mradi tayari imeshatangazwa.

b) ***Mradi wa Kuanzisha na Kuendeleza Maeneo Maalum ya Viwanda (Indurstrial Parks):*** Mradi una lengo la kuimarisha maeneo tengefu ya viwanda kwa ujenzi wa viwanda vidogo vidogo na vya kati viweze kuwa katika maeneo maalum yatakayosaidia kukuza uchumi na kutoa ajira. Hadi kufikia Machi 2025, kazi ya upelekaji wa miundombinu ya barabara, maji (Construction of water network), umeme na tehama katika eneo tengefu la Dunga zinaendelea ujenzi uko asilimia 94.

c) ***Mradi wa Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonesho Zanzibar:*** Mradi una lengo la kutoa huduma za kuimarisha sekta ya biashara na viwanda na kukuza wafanyabiashara wadogo wadogo na wa kati. Hadi

kufikia Machi 2025, Ujenzi wa miundombinu na jengo la utawala katika Kituo cha Maonesho Nyamanzi unaendelea. Kazi ya uwekaji wa vioo katika ukumbi wa Dkt. Hussein Mwinyi imekamilika, kazi ya ufungaji wa kamera za CCTV imefanyika kwa baadhi ya maeneo pamoja na uwekaji wa mfumo wa mawasiliano ya mtandao (internet) katika eneo la ukumbi wa mikutano.

**Kukuza Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii**

**41.0** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2024/2025 eneo hili limepangiwa kutekeleza programu nne (4) na miradi miwili (2) ya maendeleo ambayo itagharimu jumla ya TZS 674.6 bilioni. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025) jumla ya TZS 371.0 bilioni zimepangwa na hadi kufikia Machi 2025, TZS 226.3 bilioni sawa na asilimia 61 ya lengo la TZS 371.0 bilioni zimepatikana. Utekelezaji wa eneo hili ni kama ifuatavyo: -

a) ***Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Elimu:*** Programu hii ina lengo la kuinua viwango vya elimu kwa kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunza kwa kuimarisha miundombinu ya sekta ya elimu kiujumla ili kuwawezesha wanafunzi kupata elimu katika mazingira mazuri na viwango vya ufanisi. Hadi kufikia Machi 2025, kazi ya ujenzi wa madarasa mapya 420, (Sekondari 120 na Msingi 300) imefikia asilimia 50; madarasa 170 yalioanzishwa na wananchi (madarasa 100 Msingi na 70 Sekondari) upo katika hatua mbali mbali utekelezaji wake umefikia asilimia 45. Ujenzi wa Dakhalia katika skuli 11 ikiwemo Lumumba, Misufini, Kiwani, Paje Mtule, Fidel Castro, Maziwa Ng'ombe, Mikindani na Chwaka Tumbe unaendelea katika hatua mbali mbali za utekelezaji, pamoja na ukarabati wa skuli 100 (msingi 70 na sekondari 30) utekelezaji wake umefikia asilimia 65. Katika Ujenzi wa vyuo vitano (5) vya Amali utekelezaji wake upo katika hatua ya zabuni ya kumpata Mkandarasi kwa ajili ya kuanza ujenzi, Utanuzi wa Chuo cha Karume

(KIST) utekelezaji upo katika hatua za kuandaa michoro ya kina (detail drawings) na Mshauri Elekezi yupo katika hatua za mwisho za kukamilisha kazi hiyo. Ujenzi wa skuli tatu (Skuli ya Gamba, Mfenesini kwa Unguja na Skuli ya Kifundi kwa Pemba) zenye Dakhalia kwa mashirikiano na BADEA upo katika hatua ya kukamilisha utekelezaji wake kwa ujumla umefikia asilimia 90.

b) ***Programu ya Ukarabati na Ujenzi wa Vituo vya Afya ya Msingi:*** Programu hii ina lengo la kuimarisha afya ya msingi kwa kuimarisha miundombinu ya vituo vya afya vya msingi ili viweze kutoa huduma za afya ya msingi zenye viwango na kuimarisha afya ya jamii. Hadi kufikia Machi 2025, ujenzi wa vituo 10 vya afya ya msingi (Nungwi, Mahonda, Sebleni, Konde, Jadida, Mtambile Kiuyu, Minungwini, Chonga, Vitongoji) Ujenzi unaendelea kwa wastani wa asilimia 51.9 ya utekelezaji.

c) ***Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi katika Hospitali za Wilaya na Mkoa:*** Programu hii ina lengo la kuimarisha makaazi kwa madaktari ili waweze kufanya kazi katika mazingira mazuri yenye utulivu zaidi kwa kuongeza ufanisi na kuweza kupatikana katika maeneo ya kazi muda wote hasa wakati wa dharura. Kazi ya ujenzi katika nyumba hizi umefikia katika hatua mbali mbali: nyumba za wafanyakazi Mwera Pongwe ujenzi upo katika hatua ya kukamilisha mfumo wa maji na umeme na kumalizia kazi za nje na umefikia asilimia 95; Kitogani ujenzi umekamilika kazi inayoendelea ni ufungaji wa lifti na umefikia asilimia 96; Pangatupu ujenzi upo katika hatua kukamilisha mfumo wa maji na umeme na umefikia asilimia 91; na kwa upande wa Pemba, Kinyasini ujenzi upo katika hatua ya ukamilishaji kwa kupiga rangi na kumalizia kazi za nje na umefikia asilimia 97; na Vitongoji ujenzi upo katika hatua ya kumwaga zege kwa ajili ya ghorofa ya kwanza na umefikia asilimia 52.

**d) *Programu ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar***

Programu hii ina lengo la kusimamia huduma za usambazaji maji safi na salama kuhakikisha zinapatikana katika maeneo yote ya mijini na vijijini ili kuwawezesha wananchi kunufaika na huduma hiyo muhimu katika jamii. Kupitia Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (INDIA) katika maeneo ya Wilaya ya Magharibi "A", (Mfenesini, Masingini na Kizimbani) Magharibi "B" (Dimani na Kidutani) na Wilaya ya Kati (Jumbi- Mkorogo) pamoja na ujenzi wa jengo jipya la Ofisi ya Mamlaka ya Maji Zanzibar. Malipo kwa ajili ya Wakandarasi na Mshauri Elekezi kwa uangalizi wa mradi yamefanyika. Vile vile, Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji Mkoa wa Mjini Magharibi unaotekelezwa katika maeneo ya Welezo juu, Welezo Magharibi na Migombani. Malipo ya Mshauri Elekezi yamefanyika na maandalizi ya zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi yanaendelea.

**e)** ***Mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja:*** Programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za afya na ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa, katika hospitali ya Mnazi Mmoja ili kuiwezesha kutoa huduma nzuri na zenye kukidhi viwango vya hospitali ya Rufaa. Hadi kufikia Machi 2025, fedha zilizotumika ni kwa gharama za uendeshaji wa ofisi (Mishahara ya watendaji wa kitengo cha Uratibu na uendeshaji wa mradi). Hatua za Ujenzi zitaanza baada ya kukamilika kwa taratibu za upatikanaji wa fedha kutoka kwa Mshirika wa Maendeleo (Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi Afrika (BADEA)).

**f)** ***Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo:*** Mradi huu una lengo la kuweka mazingira mazuri ya makaazi kwa wananchi pamoja na kuweka haiba nzuri katika mandhari ya mji wa Zanzibar pamoja na kuwapatia wananchi wa Zanzibar makaazi yaliyo mazuri na kwa gharama nafuu.

Hadi kufikia Machi 2025, Upembuzi Yakinifu umekamilika. Kazi za kusafisha eneo na kujenga Ofisi kwa ajili ya kuwekea vifaa vya ujenzi inaendelea.

**Kuimarisha Utawala Bora na Uhimili**

**42.0 Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2024/2025 eneo hili limepangiwa kutekeleza miradi mitatu (3) ya maendeleo ambayo itagharimu jumla ya TZS 83.62 bilioni. Kwa kipindi cha miezi tisa Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya TZS 46 bilioni zimepangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2025, TZS 27.3 bilioni sawa na asilimia 59 ya lengo zimepatikana. Utekelezaji wa eneo hili ni kama ifuatavyo: -

a) ***Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama:*** Katika kuimarisha mazingira salama kwa wananchi na wageni katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar, Serikali imenunua vitendea kazi kwa ajili ya matumizi ya Idara Maalum za SMZ ikiwemo magari ya vikosi, sare za maafisa na wapiganaji pamoja vifaa vya usalama ambavyo tayari vimeshafungwa katika maeneo husika. Vile vile, Wizara tayari imeingia Mkataba na Mkandarasi wa Kampuni ya ROM Solution kwa ajili ya mategenezo ya Kamera za mradi wa Mji salama.

b) ***Mradi wa Ujenzi wa Mahakama za Wilaya na Mikoa:*** Kazi za ujenzi zinaendelea kwa hatua za kukamilisha ujenzi kwa hatua za uwekaji wa mifumo ya TEHAMA na umeme kwa upande wa Unguja Mahakama katika eneo la Mazizini - ujenzi umefikia asilimia 94 ya utekelezaji; Pale Kiongele - ujenzi umefikia asilimia 93; Tunguu/Binguni- ujenzi umefikia asilimia 96; na Kisakasaka – ujenzi umefikia asilimia 93. Kwa upande wa Pemba, eneo la Kinyasini- ujenzi unaendelea umefikia asilimia 77; Micheweni –ujenzi umefikia asilimia 70; na Changaweni - ujenzi umefikia asilimia 62.

c) ***Ujenzi wa Mji wa Serikali:*** Mradi una lengo la kujenga Ofisi za Serikali katika eneo la Kisakasaka ili kuweka mazingira mazuri kwa wafanyakazi ili waweze kutoa huduma kwa wananchi na kuongeza haiba ya mji wa Zanzibar. Jumla ya Kampuni saba (7) tayari zimeshajitokeza kuingia ubia na Serikali kati ya hizo Kampuni tano (5) zimeshafanya mazungumzo ya kina na Serikali na Kampuni mbili (2) zinaendelea na majadiliano. Aidha, Michoro ya awali imeandaliwa pamoja na usafishaji wa eneo.

## D. MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2025 MALENGO NA SHABAHA ZA UCHUMI JUMUISHI KWA MWAKA 2025

**43.0 Mheshimiwa Spika,** Uchumi wa Zanzibar unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.3 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 7.1 mwaka 2024 kwa kufikia malengo yafuatayo: -

i. Kuongezeka kwa uingiaji wa watalii watakaotembelea Zanzibar kwa asilimia 12.6 kutoka watalii 736,755 kwa mwaka 2024 hadi watalii 829,929 mwaka 2025;

ii. Kuendelea kutekelezwa kwa miradi mikubwa ya maendeleo ikiwemo miundombinu ya barabara za mjini na vijijini, ujenzi wa Uwanja wa Ndege Pemba, bandari ya Mangapwani na ukarabati wa bandari ya Malindi. Miradi mengine itakayoshajihisha ukuaji wa uchumi ni ujenzi wa miundombinu ya huduma za jamii ikiwemo miundombinu ya afya, elimu, maji safi na salama na ujenzi wa kiwanja kipya cha michezo - Fumba na kukamilisha viwanja vya michezo kwa kila Wilaya;

iii. Kuendelea na hatua za kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei ili kubakia katika tarakimu moja;

iv. Kuongezeka kwa uhamasishaji wa ukusanyaji wa mapato pamoja na usimamizi wa matumizi ya Serikali;

v. Kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuongeza thamani na miradi ya uwekezaji kwa Wawekezaji wa ndani na nje ya nchi;

vi. Kuongezeka kwa mchango wa sekta binafsi kutokana na juhudi za Serikali za kukuza uwekezaji, uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuongeza ajira; na
vii. Kuongezeka kwa uzalishaji katika sekta ya uchumi wa buluu na kuimarisha matumizi endelevu ya bahari baada ya kukamilika kwa ujenzi wa viwanda vya uchakataji na usarifu wa mazao ya baharini.

**44.0 Mheshimiwa Spika,** shabaha za uchumi jumla ni kama ifuatavyo:
i. Ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 7.3 mwaka 2025;
ii. Mfumuko wa bei kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya kiwango cha asilimia 5 kama ilivyo shabaha iliyowekwa kwa nchi za Afrika Mashariki;
iii. Uwiano wa Mapato ya ndani kufikia asilimia 33.4 ya Pato la Taifa mwaka 2025 kutoka asilimia 26 mwaka 2024;
iv. Uwiano wa Mapato ya kodi kufikia asilimia 33 ya Pato la Taifa mwaka 2025 kutoka asilimia 22.4 mwaka 2024;
v. Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa chini ya asilimia 3.0;
vi. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi cha miezi minne; na
vii. Kipato cha mwananchi kuendelea kubakia juu ya wastani wa Dola za Kimarekani 1,449.

**45.0 Mheshimiwa Spika,** Matarajio ya ukuaji huo yanategemea na misingi ifuatayo:
i. Kuendelea kuimarika kwa usimamizi wa sera za kifedha;
ii. Kuimarika kwa upatikanaji wa nishati ya mafuta na gesi ili kuweza kupunguza gharama za bei za nishati hizo;
iii. Kuendelea kuimarika kwa miundombinu na huduma za bandari zetu ambazo zitapunguza gharama za upatikanaji wa huduma na bidhaa muhimu;
iv. Kuwa na uwekezaji zaidi katika sekta ya viwanda ili kuongeza thamani ya bidhaa kwa matumizi ya ndani na usafirishaji nje ya nchi;

v. Kuanza kwa miradi inayotarajiwa kuwa ni nyenzo za kuwezesha Zanzibar kukaribisha timu kwa mazoezi na baadhi ya mechi za Mashindani ya kuwania Kombe la Afrika (AFCON); na
vi. Kuendelea kuwepo kwa hali ya usalama nchini na kwa nchi jirani.

**46.0 Mheshimiwa Spika,** Vile vile, Serikali itaendelea kuchukua hatua za kuweka utulivu wa bei kwa wananchi ikiwemo: -

i. Kuendelea kutoa bei elekezi na kusimamia bidhaa zinazoingia nchini zikiwemo bidhaa za chakula na vifaa vya ujenzi;
ii. Kuendelea kutekeleza Sera ya Fedha kupitia Benki Kuu ya Tanzania ili kutunza thamani ya Shilingi ya Tanzania na kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei;
iii. Kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT) Serikali itaendelea kudhibiti mwenendo wa sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine Duniani;
iv. Kuendelea kushajihisha na kuimarisha shughuli za uzalishaji viwandani;
v. Kuimarisha maghala na mifumo ya uhifadhi wa chakula ili kuwa na uhakika wa chakula nchini; na
vi. Kuendelea kutoa na kusimamia utoaji wa ruzuku hasa kwa vyakula vikuu vinavyolimwa hapa nchini.

**47.0 Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, Matarajio hayo ya ukuaji wa uchumi wa Zanzibar yanaweza kuathirika kutokana na mabadiliko ya sera za biashara za Kimataifa kutoka Marekani, ikiwemo kutorejeshwa upya (Renewed Contract) kwa Mkataba wa biashara za Kimataifa juu ya usafirishaji wa bidhaa kutoka nchi za Afrika kwenda katika soko la Marekani bila ya kutozwa ushuru kupitia Mkataba wa African Growth  Opportunity Act (AGOA) na Mkakati wa Marekani wa kuongeza ushuru kwa bidhaa zinazotoka Afrika, zikiwemo Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kuichumi Kusini mwa Afrika (SADC).

## E. MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2025/2026

**48.0** **Mheshimiwa Spika,** Mpango huu umeandaliwa kwa lengo la kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo Zanzibar 2050, ambayo ni kuiwezesha Zanzibar kuwa nchi yenye hadhi ya Uchumi wa Kipato cha Kati (Upper Middle-Income Status). Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2025/2026 umezingatia Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026 ambao unafikia mwisho wa utekelezaji wake, Utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020-2025 na Hotuba ya ufunguzi wa Baraza la 10 la Wawakilishi. Mpango huu pia umezingatia Maelekezo ya Serikali Kiujumla, ahadi zinazotolewa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa wananchi pamoja na maagizo ya viongozi wakuu wa nchi. Pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030 na Agenda za Afrika 2063.

**49.0** **Mheshimiwa Spika,** Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatarajiwa kukaribisha baadhi ya mechi za mashindano na mazoezi kwa mchezo wa mpira wa miguu wa Kombe la Nchi za Afrika (AFCON) mwaka 2027. Hivyo, miongoni mwa vipaumbele vya Mpango huu ni utekelezaji wa miradi wezeshi ili kufanikisha mashindano hayo, kuiwezesha Zanzibar kunufaika na fursa za kiuchumi, kibiashara na kijamii sambamba na kuendelea kukamilisha miradi ya kimkakati.

## D. MAPENDEKEZO YA MAENEO YA KIMKAKATI KWA MWAKA 2025/2026

**50.0** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka 2025/2026, Serikali inaendelea na Mkakati wa kuibadilisha Taswira ya Zanzibar kwa kuweka mbele maendeleo ya kiuchumi na kijamii kupitia maeneo matano ya Kimkakati kama yalivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021 – 2026 ambayo ni: **(i) Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu; (ii) Mazingira Wezeshi na Uimarishaji**

**wa Miundombinu; (iii) Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi; (iv) Kukuza Rasilimali Watu na Huduma za Kijamii; na (v) Kuimarisha Utawala na Uhimili.** Kiasi cha TZS 3,292.22 bilioni zinatarajiwa kutumika kugharamia programu na miradi ya maendeleo ya kimkakati sawa na ongezeko la asilimia 57.77 ikilinganishwa na TZS 2,086.71 bilioni za Bajeti ya Maendeleo ya mwaka 2024/25.

**i Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu**

**51.0 Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea na utekelezaji wa sera na mikakati ya kuendeleza sekta ya uchumi wa buluu kwa ujenzi wa miundombinu ya viwanda vya usarifu wa mazao ya baharini pamoja na utalii wa bahari na visiwa. Kwa mwaka 2025/2026, kiasi cha TZS 428.09 bilioni zinatarajiwa kutumika kwa kugharamia ujenzi wa miundombinu ya uvuvi na ujenzi wa bandari jumuishi ya Mangapwani, Mpigaduri na bandari ya uvuvi Shumba.

**ii. Mazingira Wezeshi na Kuimarisha Miundombinu**

**52.0 Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea na uimarishaji wa miundombinu ya usafiri wa Anga ikiwemo ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Pemba, **Ujenzi wa Jengo la Abiria la Pili katika** Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amaan Karume pamoja na kuanza ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Nungwi. Vile vile, kuendelea na ujenzi wa barabara kuu Unguja na Pemba zenye urefu wa kilomita 782.9 zikiwemo za mjini, vijijini, za ndani na zile zinazounganisha hoteli pamoja na ujenzi wa misingi/mitaro na matengenezo ya maziwa katika maeneo ya Miji.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu hii kutakuwa na uendelezaji wa kazi za ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji, na umeme na upatikanaji wa umeme wa jua. Kwa mwaka 2025/2026, Kiasi cha **TZS 1,201.42 bilioni** zitatumika kutekeleza programu na miradi hiyo.

**iii. Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi**

**53.0 Mheshimiwa Spika,** Kiasi cha TZS 148.91 bilioni zitatumika kutekeleza programu na miradi iliyoainishwa katika eneo hili.

Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu katika maeneo tengefu ya Viwanda, Biashara ili kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Vile vile, kuendeleza shughuli za uzalishaji wa mazao ya kilimo kupitia uendelezaji wa miundombinu ya uzalishaji na uhifadhi wa chakula, kushajiisha kilimo cha mazao mbadala ikiwemo viungo kwa ajili ya usafirishaji na kuanza utekelezaji wa mageuzi ya kilimo ili kukuza uzalishaji. Aidha, Serikali imedhamiria kuendelea kuimarisha miundombinu ya uchumi wa kidijitali kwa kulaza Mkonga wa Kimataifa wa Baharini Zanzibar (International Gateway); ujenzi wa Kituo cha kuhifadhia taarifa (Tier III data center); na Kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha na uendeshaji wa shughuli za Serikali.

**iv. Kukuza Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii**

**54.0** **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kijamii Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu na rasilimali watu sambamba na utoaji wa huduma zenye viwango. Katika kufanikisha hilo, Serikali inakusudia kuanza ujenzi na ukarabati mkubwa wa hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja; ujenzi wa hospitali ya Binguni ambayo itakua ni Taasisi ya tiba, tafiti na kufundishia; Ujenzi wa nyumba za bei nafuu katika maeneo ya Chumbuni, Kisakasaka, Nyamanzi, Kwahani, Mfikiwa, Mkungu Malofa na Saateni; Ujenzi wa kiwanja kipya cha Michezo – Fumba na Viwanja vya Michezo vya Wilaya. Kwa upande wa sekta ya elimu, Serikali inaendelea na ujenzi wa madarasa 1,000, Utanuzi wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) pamoja ujenzi wa dakhalia katika skuli mbali mbali Unguja na Pemba. Kiasi cha **TZS 1,260.14 bilioni** zitatumika kutekeleza programu na miradi hiyo.

**V. Kuimarisha Utawala Bora na Uhimilivu**

**55.0** **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuimarisha ulinzi na usalama pamoja na kuimarisha upatikanaji wa haki ili kuhakikisha nchi inaendelea kubaki katika hali ya utulivu na amani sambamba na uhifadhi wa Zanzibar kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Miradi itakayotekelezwa ni: kuimarisha ulinzi na usalama; Ujenzi

wa Mahkama za Wilaya na Mikoa; na Uhifadhi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi. Kiasi cha **TZS 253.65 bilioni** zinatarajiwa kutumika.

**56.0** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2025/2026 Serikali inatarajia kutekeleza miradi mengineyo ambayo itagharimu **TZS 1,247.26 bilioni.** Miradi hii inajumuisha miradi inayoendelea, miradi yenye dhima ya fedha za Serikali kwa Washirika wa Maendeleo na upelekaji wa miundombinu katika maeneo yanayotarajiwa kutekelezwa miradi ya kimkakati kama inavyoonekana katika Kitabu cha Pili.

## RASILIMALI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2025/2026

**57.0** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2025/2026, Serikali imepanga kutumia kiasi cha **TZS 4,547.96 bilioni** (**TZS 4,539.49** kwa miradi ya Serikali Kuu na **TZS 9.17 bilioni** kwa miradi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa) kwa kutekeleza shughuli za maendeleo. Mpango wa Maendeleo unategemewa kugharimu **TZS 3,231.40** bilioni kutoka Serikalini sawa na asilimia 71.20 ya Bajeti yote ya Maendeleo na **TZS 1,308.09** bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 28.80. (**TZS 962.74 bilioni** ni Mikopo na **TZS 345.35 bilioni** ni Ruzuku). Fedha hizi zitatumika kugharamia utekelezaji wa programu 41 na miradi 56 kama ilivyoainishwa katika Kitabu cha Pili **(Mwelekeo wa Hali ya uchumi wa Zanzibar 2025 na Mpango wa Maendeleo wa 2025/2026).** Aidha, Miradi mingine ya Maendeleo, itaendelea kugharamiwa na sekta binafsi kwa utaratibu wa Ushirikiano (Ubia) kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP).

## MAENEO MTAMBUKA

### Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP -2021-2026)

**58.0** **Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026 ni Mpango wa kwanza kutafsiri Dira ya Maendeleo ya

Zanzibar (ZDV) ya mwaka 2050 yenye dhamira ya kuleta mageuzi ya kiuchumi na kijamii; na kuondoa umasikini Zanzibar. Mpango huu uliandaliwa na kuanza kutumika katika Serikali ya Awamu ya Nane (8) kuanzia mwaka mwaka 2021 ukiwa na kaulimbiu isemayo "Uchumi wa Buluu kwa Ukuaji Jumuishi na Maendeleo Endelevu," kwa lengo la kujenga misingi ya kuibadilisha Zanzibar kuwa nchi ya Kipato cha Kati cha juu (Upper Middle-Income Status) ifikapo mwaka 2050. Utekelezaji wa Mpango huu unatarajiwa kukamilika mwaka 2026.

**59.0** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango kupitia Tume ya Mipango inaendelea na Tathmini ya Mpango huo kwa kuzingatia maeneo mbali mbali ya utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo ikiwemo ya Kimkakati. Tathmini hii itaonesha mafanikio na changamoto. Mafanikio yataendelezwa ili kuwa na uchumi endelevu na changamoto zitafanyiwa kazi zigeuke kuwa fursa katika kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050.

**Masuala ya Idadi ya Watu**

**60.0** **Mheshimiwa Spika,** Idadi ya watu Zanzibar ni kiashiria muhimu cha kuweza kupanga mipango ya maendeleo pamoja na utoaji wa huduma kwa wananchi. Kwa mwaka 2022, matokeo ya Sensa ya Watu na Makaazi yanaonesha kuwa Zanzibar ina jumla ya watu 1,889,773 (wanaume 915,492 na wanawake 974,281). Vile vile, kasi ya ukuaji wa Idadi ya watu imefikia asilimia 3.7 kwa mwaka 2022 kutoka asilimia 2.8 mwaka 2012. Aidha, kiwango cha watu wanaoishi katika eneo kwa kila kilomita moja ya mraba (population density) kimeongezeka kutoka watu 530 mwaka 2012 hadi watu 768 kwa mwaka 2022. Katika kuzingatia takwimu hizo, Ofisi ya Rais- Fedha na Mipango kupitia Tume ya Mipango imeandaa Rasimu ya Sera ya Idadi ya Watu inatarajiwa kutoa mwongozo wa kuoanisha viashiria vya masuala ya idadi ya watu katika mipango ya maendeleo na bajeti. Aidha, Serikali imejipanga kuandaa ripoti inayohusu mgawanyo wa idadi ya watu na faida

zake (Zanzibar Demographic Dividend Report); Kuingiza taarifa za Kaya kwa kutumia mfumo wa Daftari la Shehia (Shehia register) ambao unatumia mfumo wa taarifa za Kijografia (Geographical Information System (GIS)).

**Uhifadhi wa Mazingira**

**61.0** **Mheshimiwa Spika,** Katika kulinda na kuhifadhi mazingira pamoja na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, Serikali ilifanikiwa kujenga ukuta wenye urefu wa mita 70 katika eneo la Kisiwa Panza – Pemba ambao umesaidia kuzuia maji ya chumvi kuingia katika maeneo ya kilimo na makaazi ya wananchi; Kuunganishwa kwa nyumba (Kaya) 147 katika mfumo wa kudhibiti maji machafu katika eneo la Msingini Chake Chake – Pemba ili kudhibiti maradhi ya kuambukiza kutokana na kusambaa kwa maji machafu katika baadhi ya maeneo ya jamii; na Kufanya tathmini ya sekta 10 hatarishi (Vulnerability Assesment of Sectors) zinazoathirika na mabadiliko ya tabianchi zikijumuisha sekta ya utalii, afya, kilimo, misitu, mifugo, mawasiliano, ardhi, nishati, uvuvi na uchumi wa buluu kwa ajili ya kuziwezesha sekta hizo kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

**62.0** **Mheshimiwa Spika,** Serikali imepanga kufanya utafiti wa kutambua maeneo yalioathirika na mabadiliko ya tabianchi pamoja na kufanya utafiti wa mabwawa ya asili na michirizi ya maji katika maeneo kwa Pemba; pamoja na kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Kuirithisha Zanzibar ya Kijani ili kuimarisha hali ya uasili wake kwa kuendeleza maeneo yaliyoharibiwa kimazingira Unguja na Pemba. Vile vile, kuhakikisha kuwa miradi yote ya maendeleo inafanyiwa Upembuzi Yakinifu juu ya athari za kimazingira ili kuifanya miradi hiyo kuwa endelevu na bila ya kuleta uharibifu na uchafuzi wa mazingira; na kuendelea kuhamasisha jamii juu ya uhifadhi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuimarisha uhimili wa athari za mabadiliko ya tabianchi.

### Kukabiliana na Maafa

**63.0** **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa imekua ikichukua juhudi za kudhibiti na kupunguza athari zinazotokana na Maafa ikiwemo kufanya Mapitio ya Mpango Mkakati wa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa wa Mwaka 2019-2024 na kupatikana kwa Mpango Mkakati mpya wa Mwaka 2024-2029 ili kukidhi vigezo vya kutoa huduma wakati wa maafa. Vile vile, kuimarisha Mfumo wa Taarifa za Maafa (Zanzibar Disaster Management Information System) pamoja na kutoa mafunzo ya masuala ya Maafa kwa wanafunzi 5,500 wa skuli za Msingi 55 (35 Unguja na 20 Pemba). Kwa mwaka 2025/2026 Serikali itaendelea kuimarisha zaidi Mfumo wa Taarifa za Maafa Zanzibar na kusambaza taarifa za tahadhari za mapema kwa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi.

### Mapambano dhidi ya dawa za kulevya

**64.0** **Mheshimiwa Spika,** Katika juhudi za kupambana na kudhibiti dawa za kulevya, Operesheni za kuwakamata wahalifu wa dawa za kulevya zimekua zikifanyika. Kupitia operesheni hizo, kesi 107 (89 Unguja, 18 Pemba) zilifunguliwa, watuhumiwa wa kesi za dawa za kulevya wamefikishwa katika vyombo vya Sheria na kuwafungulia kesi Mahakamani, kesi 72 (kesi 49 Huru na kesi 23 Hatia) zimetolewa hukumu na kesi 171 bado zinaendelea Mahakamani. Elimu inaendelea kutolewa kwa jamii juu ya athari na madhara ya dawa za kulevya kwa taasisi za elimu, masheha, wananchi, vikosi vya Ulinzi na Usalama na maeneo ya kazi kwa Unguja na Pemba. Jumla ya wanafunzi 7,343 (wanaume 3,228 na wanawake 4,115) na walimu 71 walipatiwa elimu hiyo. Serikali imepanga kujenga Kituo cha Marekebisho ya Tabia Pemba pamoja na kufanya Operesheni kubwa na za kawaida katika maeneo mengi ya Unguja na Pemba sambamba na kuendelea na kutoa taaluma na hamasa kwa jamii kuhusiana na athari za matumizi ya dawa za kulevya.

**Makundi yenye Mahitaji Maalumu**

**65.0** **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu limeweza kukamilisha Mfumo wa Jumuishi Kielektroniki wa Kuhifadhia Taarifa za Watu Wenye Ulemavu (Jumuishi Management Information System) pamoja na kufanya ziara ya kuvitembelea vikundi 43 vya ujasiriamali vya Watu wenye Ulemavu, ili kuvihamasisha vikundi hivyo juu ya masuala ya kuomba mkopo wa 4 - 4 - 2 unaotolewa na Halmashauri kupitia Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Vifaa saidizi 105 vikiwemo vya magurudumu mawili 55 (wanaume 28 na wanawake 27) na Fimbo nyeupe 50 (wanaume 21 na wanawake 29) vyenye thamani ya TZS 27.5 milioni vimetolewa kwa Watu wenye Ulemavu. Vile vile, Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu limefanikiwa kulipia gharama za masomo ya muda mfupi na muda mrefu kwa wanafunzi wenye ulemavu kwa fani mbali mbali. Jumla ya wanafunzi 97 wenye ulemavu wamelipiwa gharama za masomo (wanaume 46 na wanawake 51). Aidha, maadhimisho ya siku ya Kimataifa ya Watu wenye Ulemavu Duniani yamefanyika tarehe 3 Disemba 2024, katika viwanja vya Gombani ya Kale Wilaya ya Chake Chake Pemba. Kwa mwaka 2025/26, Serikali imepanga kutoa uelewa wa masuala ya Watu wenye Ulemavu kwa jamii ambazo mwamko wake sio mkubwa na kuendelea kutafuta misaada na vifaa saidizi kwa mujibu wa mahitaji.

**Watu wanaoishi na virusi vya ukimwi (VVU)**

**66.0** **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Tume ya Ukimwi inaendelea kupunguza kasi ya maambukizi ya UKIMWI kwa kutumia mikakati na programu tafauti, katika jitihada hizo Serikali imeweza kupunguza maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI kutoka watu 255 waliopata maambukizi mapya mwaka 2023 hadi watu 211 kwa mwaka 2025. Kupunguza vifo vinavyotokana na maradhi ya UKIMWI kutoka vifo 182 mwaka 2023 hadi 115 mwaka 2025. Serikali kupitia Tume ya Ukimwi imejipanga kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano na Utetezi wa UKIMWI kwa vijana, kuratibu

utekelezaji wa Mkakati wa Nne wa Taifa wa UKIMWI ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na kuhakikisha miradi ya maendeleo inazingatia masuala ya UKIMWI ili kudhibiti maambukizi mapya ya VVU.

**Mipango ya Kuendeleza Watenda Kazi**

**67.0 Mheshimiwa Spika,** Uwekezaji katika Rasilimali watu kwa kupata wanataaluma na wenye ujuzi ni jambo muhimu sana. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuimarisha masuala ya rasilimali watu ili kuleta tija na manufaa katika jamii. Katika kufanikisha hilo, Ofisi ya Rais- Fedha na Mipango kupitia Tume ya Mipango ilishirikiana na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ya Zanzibar kutoa muongozo wa vipaumbele vya elimu vya Taifa utakaowasaidia wanafunzi kupata mikopo ya elimu ya juu; kutoa uwelewa kwa wanafunzi wa skuli za sekondari juu ya fani za kipaumbele pamoja na kuandaliwa kwa mfumo wa wahitimu Zanzibar (Zanzibar Graduate Tracking System). Kwa mwaka 2025/2026, Tume ya Mipango inakusudia kuandaa Kanzidata ya Rasilimali Watu (HR Database) ikizingatia sifa na wataalamu waliopo na wanaohitajika na kuandaa muongozo wa mafunzo kwa vitendo (Zanzibar Internship Guidelines).

**UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI**

**68.0 Mheshimiwa Spika,** Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo ni moja ya nyenzo muhimu inayopima ufanisi wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo kwa kubainisha mafanikio na changamoto. Tume ya Mipango inaendelea kutumia mbinu za Ufuatiliaji, Tathmini na Kuripoti kwa kutumia viashiria vilivyoainishwa katika Muongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP M&E Framework) 2021–2026 ili kupima utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo na kuchukua hatua stahiki za kufikia malengo ya utekelezaji kwa muda uliopangwa. Miongozo

ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango inayozingatia Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 na Sheria ya Fedha ya mwaka 2016, inaendelea kuzingatiwa.

**69.0** **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Malengo na Mikakati ya Maendeleo Kikanda na Kimataifa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 17, kwa mwaka 2024/25 Zanzibar inaendelea na maandalizi ya Ripoti ya utekelezaji wa SDGs na itawasilisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hatimae kuwasilishwa Umoja wa Mataifa, katika Mkutano wa Jukwaa la Siasa la ngazi za juu unaofanyika kila mwaka. Kwa mwaka 2024/25 Malengo yaliyopewa mkazo zaidi ni Malengo matano (5): **Lengo nambari 3,** Kuhakikisha uwepo wa Afya na maisha mazuri kwa watu wote na rika zote; **Lengo Nambari 5,** Kuwepo na usawa wa Kijinsia na Kuwezesha Wanawake na Wasichana; **Lengo Nambari 8,** Ukuaji wa Uchumi Endelevu, Jumuishi na Ajira zenye staha kwa wote; **Lengo Nambari 14**, Kuhifadhi na Kutumia rasilimali za bahari kwa njia endelevu kwa Maendeleo Endelevu na **Lengo nambari 17,** Kukuza Ushirikiano wa Kimataifa kwa Maendeleo Endelevu. Kwa upande wa utekelezaji wa Ajenda za Afrika 2063 (African Agenda 2063) utekelezaji wake unakwenda sambamba na Malengo ya Maendeleo Endelevu. Mafanikio katika kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na Ajenda za Afrika yanaonekana katika Programu na Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Serikali ambayo imeanza kuleta tija kwa wananchi kwa kukuza uchumi na ustawi wa jamii. Kazi ya matayarisho ya uandaaji wa Ripoti ya Hiari ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu kwa ngazi za Mikoa inaendelea na inatarajiwa kuwasilishwa Serikalini baada ya kukamilika. Ripoti hizi zitajumuisha Mikoa yote ya Zanzibar kwa kukusanya taarifa za utekelezaji wa Programu na miradi ya maendeleo inayotekelezwa na kusimamiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**70.0** **Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia umuhimu wa Ufuatiliaji na Tathmini, Tume ya Mipango inakamilisha Rasimu ya Sera ya

Ufuatiliaji na Tathmini kwa ajili ya kutoa muongozo na kusimamia maswala yote yanayohusu Ufuatiliaji na Tathmini nchini. Sera hiyo ipo katika ngazi za kimaamuzi kwa kupata ridhaa kwa ajili ya kuanza kutumika. Aidha, mafunzo ya uelewa wa Sera hiyo yatatolewa kwa Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na sekta binafsi ili kila Sekta ifahamu na kuweza kuitumia kwa maendeleo ya dhana ya Ufuatiliaji na Tathmini nchini na hatimae kuleta uwajibikaji katika kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo.

**71.0** **Mheshimiwa Spika,** katika kufanikisha shughuli za Ufuatiliaji na Tathmini katika utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo, Tume ya Mipango Zanzibar imefanikisha Zanzibar kuwa mwenyeji wa Kongamano la Kitaifa la Wiki ya Ufuatiliaji, Tathmini na Kujifunza (MEL WEEK) lililofanyika Septemba 2024. Kongamano hili la siku tano (5) hufanyika kila mwaka hapa Tanzania lina lengo la kuendeleza juhudi za Serikali za Kujenga Uelewa na Utamaduni wa Ufuatiliaji na Tathmini kwa Watendaji wa Serikali, Taasisi Binafsi, Asasi za Kiraia, Washirika wa Maendelo na Jamii kwa ujumla. Vile vile, kongamano hilo linashajihisha utalii kwa kuhudhuriwa na wageni kutoka katika mataifa mbali mbali.

**72.0** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha uwezo wa maafisa Ufuatiliaji na Tathmini katika Taasisi zote za Serikali, Tume ya Mipango inaendelea na kutafuta ufadhili kwa Washirika wa Maendeleo kwa lengo la kuzijengea uwezo Taasisi kiutendaji ili kutumia miongozo ya Ufuatiliaji, Tathmini na Kuripoti Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo. Tume ya Mipango Zanzibar, inaendelea kuwakaribisha Watendaji kutoka Taasisi za Serikali na Binafsi wanaotaka kujengewa uwezo katika shughuli za Ufuatiliaji na Tathmini kama inavyofanywa na baadhi ya Taasisi zinazoleta watendaji wao ili kujengewa uwezo.

## MAJUMUISHO

**73.0 Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2025/2026 ni moja kati ya njia ya kuelekea uchumi wa kati katika kipato cha juu kama ilivyo dhamira na tunu ya Wazanzibari, unaolenga kuimarisha maisha bora, amani, utulivu, utawala bora, jamii iliyoelimika, afya bora na kuwa na uchumi shirikishi na shindani. Kwa kutambua mchango na umuhimu wa sekta binafsi, Mpango huu umeipa sekta binafsi umuhimu wa kipekee kuweza kufanyakazi kwa mashirikiano na Serikali. Serikali itaendelea kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuongeza miradi shirikishi (PPP) katika kugharamia utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo.

**74.0 Mheshimiwa Spika,** naomba nimalizie kwa kusisitiza kuwa utekelezaji wa Mpango huu unamhusu kila mmoja wetu, hivyo mashirikiano katika kila ngazi ni muhimu ili kufikiwa malengo yetu ya kukuza uchumi wa Zanzibar. Ni jambo muhimu kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika kutoa maoni na kutekeleza miradi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu sambamba na uwajibikaji ndani ya utumishi wa umma. Naomba pia, nitoe wito kwa kila sekta kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa zinatekelezwa ipasavyo katika eneo lake la kiutendaji.

## HITIMISHO

**75.0 Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati na kwa niaba ya Serikali ninaomba kutumia fursa hii adhimu ya kuwashukuru wadau wote wa maendeleo wakiwemo Waheshimiwa Wawakilishi, Wabunge, Madiwani, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia, Taasisi za Dini, Washirika wa Maendeleo na Wananchi kwa ujumla kwa ushirikiano wao katika mipango, utekelezaji na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo na kujenga uchumi wa nchi yetu. Ushiriki wao wa dhati umewezesha kupatikana kwa mafanikio makubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ninawaomba waendelee kutupa ushirikiano katika kutekeleza Mpango huu ili kufikia malengo tuliyojiwekea.

**76.0 Mheshimiwa Spika,** Naomba niwatambue Washirika wa Maendeleo wa ndani kwa Mwaka 2025/2026 kama ifuatavyo: PBZ, ZSSF, ZANZIBAR MILELE FOUNDATION, ZANZIBAR MAISHA BORA FUNDATION, MWANAMKE INITIATIVE FOUNDATION, NMB, NBC, CRDB na COSTECH. Kwa upande wa Washirika wa Maendeleo wa nje na nchi rafiki zinazoendelea kushirikiana nasi kwa mwaka 2025/2026 ni pamoja na ACRA, AF, AFD-FRANCE, AfDB, AMREF, AUSTRIA, BADEA, BELGIUM, CHINA, (CIDA) CANADA, DANIDA, DfID, EDF, EU, EXIM BANKS za India, China na Korea, FAO, FINLAND, GAVI, GEF, GLOBAL FUND, GERMANY (GIZ AND KfW), GPE, GOOD NEIGHBOURHOOD, HIPZ, IAEA, INDIA, IFAD, ILO, IMF, IRELAND, JAPAN (JICA), KHALIFA FUND, MFUKO WA MAENDELEO WA UMOJA WA FALME ZA KIARABU (UAE), KOREA, KUWAIT, MALAYSIA, NORWAY, OMAN, OPEC FUND, PMI, QATAR CHARITY ORGANISATION, SAUDI FUND, SAVE THE CHILDREN, SIDA, STBF, SWEDEN, THPS, TfT, UK, UKEF/CITI BANK NA DEUTCH BANK, UN, UNDP, UNEP, UNFPA, UNESCO, UNICEF, UNIDO, USAID, UN WOMEN, UTURUKI, WORLD BANK na WHO. Kipekee naomba nitoe shukrani kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kushirikiana na Zanzibar katika utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo.

**77.0 Mheshimiwa Spika,** Kabla ya kumaliza Hotuba yangu hii naomba nitoe shukrani za dhati kwa Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango Mheshimiwa Juma Makungu Juma ambaye ni msaidizi wangu wa karibu kwa umakini wake, busara na weledi katika kutekeleza majukumu ya kazi zetu. Pia, nawashukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Mawaziri, Naibu Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Idara zinazojitegemea, Taasisi na Mashirika ya Umma kwa ushirikiano wao katika maandalizi ya Hotuba hii. Aidha, natoa shukrani za dhati kwa Makatibu Wakuu wa Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Watendaji wao wakiongozwa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi Mhandisi Zena Ahmed Said kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika matayarisho ya Hotuba hii. Mashirikiano haya yanazidisha nguvu

na kasi ya utekelezaji wa Mipango yetu ya Maendeleo sambamba na ufuatiliaji wa karibu wa malengo ili kupata matokeo yenye tija kwa wananchi.

**78.0** **Mheshimiwa Spika,** Shukrani za dhati na za kipekee naomba kuzitoa kwa watendaji wote wa Tume ya Mipango wakiongozwa na Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Dkt. Rahma Salim Mahfoudh kwa umakini na ushirikiano wao katika hatua zote hadi kupatikana kwa Hotuba hii. Niwashukuru pia, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais -Fedha na Mipango Dkt. Juma Malik Akil, Naibu Katibu Mkuu CPA. Aboud Hassan Mwinyi na Mhasibu Mkuu wa Serikali CPA. Hamad Saleh Hamad kwa kuendelea kufanya kazi kwa karibu na Tume ya Mipango. Nawashukuru Makamishna wote wa Tume ya Mipango akiwemo Ndugu Mohamed Masoud Salim Kamishna wa Idara ya Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Kisekta, Dkt. Zuhura Mohamed Abdalla Kamishna wa Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini, Dkt. Ameir Haji Sheha Kamishna Idara ya Ukuzaji Uchumi, Dkt. Afua Khalfan Mohamed Kamishna wa Idara ya Utafiti na Dkt. Rukayya Wakif Mohamed Kamishna wa Idara ya Maendeleo ya Watendakazi.

**79.0** **Mheshimiwa Spika,** Kwa vile mwaka huu tunafanya Uchaguzi tunazidi kumuomba Allah atuwezeshe kufanya maandalizi mazuri ya Uchaguzi, huduma bora wakati wa Uchaguzi na mashirikiano mema baada ya Uchaguzi. Amani na utulivu viwe ngao yetu katika Uchaguzi wetu na dira ya kutekeleza masuala mbali mbali ya maendeleo.

**80.0** **Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii inaambatanishwa na vitabu vya Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2024 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2024/2025 na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar 2025 na Mpango wa Maendeleo wa 2025/2026 ambavyo vina taarifa na uchambuzi wa kina, vinapatikana pia katika tovuti ya Tume ya Mipango (http. planningznz.go.tz).

81.0 **Mheshimiwa Spika,** Naomba sasa Baraza lako Tukufu lipokee na kujadili Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2025/2026 wenye kugharimu kiasi cha TZS 4,539.49 bilioni.

82.0 **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima naomba kutoa hoja.

**DKT. SAADA MKUYA SALUM**
**WAZIRI WA NCHI,**
**OFISI YA RAIS–FEDHA NA MIPANGO,**
**ZANZIBAR.**